TANGAZO LA SERIKALI Na. 811 la tarehe. 13/9/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa baiskeli, mkokoteni, au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"maegesho" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnara" maana yake ni kifaa kinachopokea na kusafirisha mawasiliano ya simu au redio isipokua mnara unaotumika kuongoza vyombo vya usafiri;

"soko", "gulio" au "mnada" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua bidhaa au huduma kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri; na

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atapaswa kulipa ada au ushuru husika kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1).

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kwa kuzingatia makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa chini ya Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ukusanyaji wa madeni

7.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ya (3) na (4), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

8.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa ajili ya kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

9.-(1) Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri baada ya muda ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1) kupita katika maeneo ambayo huduma au biashara inafanyika kwa saa ishirini na nne.

Makosa

10.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) anashindwa, anadharau, anakwepa au anakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) anamshawishi mtu au kikundi cha watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) anamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) anatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;

(e) anashindwa kutoa taarifa sahihi au anatoa taarifa za

uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;

(f) anashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(g) anatengeneza, anatayarisha, anaidhinisha kutengeneza au anatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri; au

(h) anatumia chombo chochote cha usafiri kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

Adhabu

11. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa lolote kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS. Na. 278 la 2017

13. Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri Wilaya ya Ludewa ya Mwaka 2017 inafutwa.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

SEHEMU A: ADA YA MATANGAZO YA BIASHARA

| Na. | Aina ya Tangazo | Kiwango cha Ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Maombi ya kuweka bango la biashara | 10,000/= kwa kila ombi |
| 2 | Matangazo yanayong'aa kwa nguvu ya umeme kwa mita ya mraba | 15,000/= kwa mwaka |
| 3 | Ubao wa tangazo usioanganza/kung'aa kwa mita ya mraba | 10,000/= kwa mwaka |
| 4 | Bango la tangazo lililoangaza au kung'aa kwa mita ya mraba | 10,000/= kwa mwaka |
| 5 | Tangazo la kutumia kitambaa | 30,000/= kwa siku |
| 6 | Tangazo la karatasi | |
| | a) Ukubwa wa A4 | 1,000/= kwa siku |
| | b) Ukubwa wa A3 | 1,200/= kwa siku |
| | c) Ukubwa wa zaidi ya A3 | 1,500/= kwa siku |
| 7 | Matangazo ya ukutani kwa mita ya mraba | 20,000/= kwa mwaka |
| 8 | Matangazo ya kutumia vyombo vya usafiri na vipaza sauti | 30,000/= kwa siku |
| 9 | Bango la tangazo linalobadilika badilika | 200,000/= kwa mwaka |
| 10 | Matngazo kwa njia ya maonesho | |
| | a) Kutambulisha na kuuza bidhaa | 10,000/= kwa siku |
| | b) Kutambulisha huduma | 10,000/= kwa siku |

SEHEMU B:
I: ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

| Na | Magari na vifaa vingine | Kiwango cha ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Isuzu yenye uwezo wa kubeba tani 7 | 3,000/= kwa kilometa |
| 2 | *Land cruiser hard top* | 2,000/= kwa kilometa |
| 3 | *Land cruiser pick up* | 2,000/= kwa kilometa |
| 4 | Pikipiki | 20,000/= kwa siku |
| 5 | Trekta | 200,000/= kwa siku |
| 6 | Kukodi boti | 200,000/= kwa siku |
| 7 | Vifaa vya GPS, darubini, spika, Kamera, projector na vifaa vingine vya kielektroniki. | 50,000/= kwa kifaa kwa siku |
| 8 | DGPS RTK | 300,000/= kwa siku |
| 9 | Kukodi viti vya Halmashauri | 500/= kwa kiti kimoja |
| 10 | Mashine ya kupukuchua mahindi | 1,000/= kwa gunia moja |

| | | |
|---|---|---|
| | | la kilo 90 |

II: MAJENGO NA VIBANDA VYA HALMASHAURI

| Na | Aina ya Jengo | Kiwango cha ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ukumbi mkubwa wa Halmashauri kwa sherehe | 500,000/= kwa siku |
| 2 | Ukumbi mkubwa wa Halmashauri kwa semina/warsha | 200,000/= kwa siku |
| 3 | Ukumbi mdogo wa HIMA | 100,000/= |
| 4 | Kupangisha eneo la umma kusimika mnara wa simu na huduma nyingine. | 300,000/= kwa mwezi kwa eneo la ukubwa usiozidi mita 5 za mraba. |
| 5 | Nyumba za Halmashauri daraja I | 80,000/= kwa mwezi |
| 6 | Nyumba za Halmashauri daraja II | 50,000/= kwa mwezi |
| 7 | Nyumba za Halmashauri daraja III | 30,000/= kwa mwezi |

SEHEMU C:
ADA NA USHURU WA SOKO NA MNADA

| Na | Aina ya ushuru | Kiwango cha ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa meza sokoni | 500/= kwa siku |
| 2 | Ushuru wa mnada /Lembuka | 500/= kwa siku |
| 3 | Ushuru wa kuingiza gari la mizigo sokoni | |
| | Tani 1 hadi 3 | 1,000/= kwa siku |
| | Zaidi ya tani 3 | 2,000/= kwa siku |
| 4 | Ushuru wa choo sokoni | 200/= |

SEHEMU D:
ADA YA HUDUMA YA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

| Na | Ada ya machinjio na Ukaguzi wa nyama | Kiwango cha Ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila ng'ombe anayechinjwa | 9,000/= kwa ng'ombe |
| 2 | Ada ya machinjio na ukaguzi wa nguruwe, kondoo na mbuzi | 7,000/= kila mmoja |
| 3 | Kuwamba na kukausha ngozi eneo la machinjio | |
| | Ng'ombe | 500/= kwa kipande kwa siku |
| | Mbuzi, kondoo | 200/= kwa kipande kwa siku |
| 4 | Ushuru wa bucha | 7,000/= kwa siku |

SEHEMU E:
USHURU WA MIFUGO NA BIDHAA KWENYE MNADA WA MIFUGO

| Na | Aina ya Mfugo | Kiwango cha Ushuru (shilingi) |
|---|---|---|

*Tangazo la serikali Na.811 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe au Punda | 5,000/= kwa kila mmoja |
| 2 | Nguruwe | 1,500/=kwa kila mmoja |
| 3 | Mbuzi au Kondoo | 1,500/=kwa kila mmoja |
| 4 | Kuku au Bata kwa tenga lenye idadi ya 5 | 1,000/= |
| 5 | Ushuru wa ngozi ya Ng'ombe au Punda | 500/= kwa kipande |
| 6 | Ushuru wa ngozi ya mbuzi au kondoo | 250/= kwa kipande |
| 7 | a) Tenga la kuku | 3,000/= kwa tenga zaidi ya kuku 10 kila tenga. |

| Na. | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ada na Ushuru (Asilimia) |
|---|---|---|
| 1 | Viazi | 3% ya bei ya kununulia |
| 2 | Kabichi | 3% ya bei ya kununulia |
| 3 | Karoti | 3% ya bei ya kununulia |
| 4 | Ufuta | 3% ya bei ya kununulia |
| 5 | Mchele | 3% ya bei ya kununulia |
| 6 | Maharage | 3% ya bei ya kununulia |
| 7 | Kahawa iliyokobolewa | 3% ya bei ya kununulia |
| 8 | Pareto | 3% ya bei ya kununulia |
| 9 | Vitunguu swaumu | 3% ya bei ya kununulia |
| 10 | Vitunguu maji | 3% ya bei ya kununulia |
| 11 | Nyanya | 3% ya bei ya kununulia |
| 12 | Mahindi/Alizeti/ngano/Mtama | 3% ya bei ya kununulia |
| 13 | Mazao mengine yasiyotajwa | 3% ya bei ya kununulia |

## SEHEMU G:
## I: ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI

| Na | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Washereheshaji | 15,000/= kwa siku |
| 2 | Wapambaji wa kumbi za burudani (harusi, sherehe za jikoni, sherehe za kuaga binti na nyinginezo) | 15,000/= kwa siku |
| 3 | Mtoa burudani (DJ)/Muziki | 15,000/= kwa tukio |
| 4 | Wamiliki wa kumbi mbalimbali | Ukumbi unaochukua watu 100-200 shilingi 20,000/=kwa siku. Ukumbi unaochukua watu 300-500 shilingi 40,000/= kwa siku. |

*Tangazo la serikali Na.811 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Matangazo ya barabarani ya sherehe | 30,000/= kwa tukio moja kwa siku |
| 6 | Mpishi wa vyakula | 30,000/= kwa tukio moja kwa siku |
| 7 | Picha jongevu na mnato | 15,000/= kwa tukio moja kwa siku. |
| 8 | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei (promotion) | 30,000/= kwa tangazo |
| 9. | Maombi ya kibali cha kufanya Tiba za Jadi | 20,000/= kwa siku |
| 10. | Matamasha | 30,000/= kwa tamasha |
| 11. | Mnada | 30,000/= kwa mnada |
| 12. | Kibali cha kupiga muziki ukumbi mkubwa | 50,000/= kwa siku |
| 13. | Kibali kupiga muziki ukumbi mdogo | 30,000/= kwa siku |
| 14. | Ngoma za jadi | 15,000/= kwa siku |
| 15. | Kibali kwa ajili ya sherehe (harusi, sendoff na matamasha) | 30,000/= kwa kibali |
| 16. | Kibali cha kuchezesha mchezo wa snuka (pooltable) | 80,000/= kwa mwaka |
| 17. | Kibali cha kuchezesha mechi za mipira | 20,000/= kwa ligi |
| 18. | Ada ya Waganga wa Jadi waliosajiliwa | 100,000/= kwa mwaka |
| 19. | Wauza dawa za asili/kienyeji | 20,000/= kwa mwaka |

II: ADA NA USHURU WA KUENDESHA SHUGHULI ZA MICHEZO YA KUBAHATISHA

| Na | Aina ya Mchezo | Kiwango cha Ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Bahati nasibu | 20,000/= kwa siku |
| 2 | Fete | 20,000/= kwa siku |
| 3 | Mashine ya kubetisha au gulugulu | 30,000/= kwa mwaka kwa mwezi |
| 4 | Ada ya leseni ya mashine ya kubetisha | 300,000/= kwa mwaka |

SEHEMU H:

I: USHURU WA MAEGESHO YA VYOMBO VYA USAFIRI STENDI, SOKONI, MWALO NA KARAKANA YA HALMASHAURI

| Na | Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Pikipiki | 300/= kwa siku |
| 2 | Teksi | 1,000/= kwa siku |
| 3 | Gari yenye uwezo wa kubeba chini ya tani 7 | 2,000/= kwa siku |

*Tangazo la serikali Na.811 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Gari yenye uwezo wa kubeba zaidi ya tani 7 | 2,500/= kwa siku |
| 5 | Mitambo | 3,000/= kwa siku |
| 6 | Bajaji, guta na pikipiki ya magurudumu matatu | 300/= kwa siku |
| 7 | Boti, Mtumbwi au chombo chochote cha uvuvi | 1,000/= kwa siku |

II: USHURU WA KUINGIZA GARI STENDI NA SOKONI

| Na | Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Pikipiki | 300/= ambaye hana stika kwa siku |
| 2 | Teksi | 500/= kwa siku |
| 3 | Gari chini ya tani 7 | 1,000/= kwa siku |
| 4 | Gari zaidi ya tani 7 | 1,500/= kwa siku |
| 5 | Magari mengine ya | 500/= kwa siku |

SEHEMU I:
I: ADA YA KUPIMA AFYA WAHUDUMU

| Na. | Aina ya Huduma | Kiwango cha ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za starehe (vilabu vya pombe za kienyeji, nyumba za kulala wageni, migahawa | 5,000/= kila baada ya miezi sita kwa kila mhudumu |
| 2 | Maduka ya bidhaa na mama lishe na baba lishe, wauza vyakula aina yoyote kwa matumizi ya binadamu na wachoma nyama, chipsi na mishkaki. | 5,000/= kila baada ya miezi sita kwa kila mhudumu |

II: ADA YA UKAGUZI

| Na. | Aina ya ukaguzi | Kiwango cha Ada (shilingi) |
|---|---|---|
| | Maombi ya ukaguzi wa kufungua au kufunga biashara | 10,000/= kwa ombi |
| | Ukaguzi wa viwanda vikubwa chenye mtaji zaidi ya Tzs.500,000,000/= | 150,000/= kwa mwaka |
| | Ukaguzi wa viwanda vya kati chenye mtaji zaidi ya Tzs.100,000,000/= hadi Tzs.500,000,0000/= | 100,000/= kwa mwaka |
| | Ukaguzi wa viwanda vidogo chenye mtaji usiodizi 100,000,000/= | 50,000/= kwa mwaka |
| | Ukaguzi wahudumu wa vyakula katika hoteli, bar na glocery | 5,000/= kila baada ya miezi sita kwa kila mhudumu |

SEHEMU J:
ADA NA USHURU WA MAZAO YA MALIASILI

| Na | Aina ya Zao | Kiwango cha Ada na Ushuru (shilingi) |
|---|---|---|

*Tangazo la serikali Na.811 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa mbao (kwa size na aina zote) | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 2 | Mkaa | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 3 | Nguzo za kujengea (dbh0-6) | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 4 | Nguzo za kujengea (dbh 7-10) | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 5 | Nguzo za kujengea zaidi ya dbh 11 | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 6 | Magogo ya kuchana mbao | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 7 | Ushuru wa kuni za matumizi ya nyumbani na viwandani kuanzia tani 1 | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 8 | Bei ya kuuza nguzo kutoka mashamba ya Halmashauri (shilingi) | |
| | a) Nguzo ya unene wa dbh 0-10 | 7,000/= kwa nguzo moja |
| | b) Nguzo ya unene wa dbh 11-20 | 20,000/= kwa nguzo moja |
| | c) Nguzo ya unene wa dbh 21-30 | 30,000/= kwa nguzo moja |
| | d) Nguzo ya unene zaidi ya dbh 30 | 40,000/= kwa nguzo moja |
| 9 | Bei kuuza miti kutoka shamba la Halmashauri (shilingi) | |
| | a) Mti wenye ujazo wa sm10-20 | 4,050/= kwa mti mmoja |
| | b) Mti wenye ujazo wa sm21-25 | 8,100/= kwa mti mmoja |
| | c) Mti wenye ujazo wa sm26-30 | 20,260/= kwa mti mmoja |
| | d) Mti wenye ujazo wa sm31-35 | 35,050/= kwa mti mmoja |
| | e) Mti wenye ujazo zaidi ya sm36 | 38,900/= kwa mti mmoja |
| 10 | Ushuru wa asali | 200/= kwa lita moja |
| 11 | Ushuru wa nta | 150/=kwa kilo 1 |
| 12 | Ushuru gundi ya miti na maganda ya miti | 100/= kwa kilo moja. |
| 13 | Tozo ya ada kwa mazao ya miti ya asili inayovunwa kwenye misitu ya hifadhi na ardhi ya kawaida kwa $M^3$ isipokuwa miti ya sandal. | |
| | i) Daraja IA | 36.000/= |
| | ii) Daraja IB | 32,000/= |
| | iii) Daraja II | 24,000/= |
| | iv) Daraja III | 18,000/= |
| | v) Daraja la IV | 12,000/= |
| | Miti mingine ambayo haijatajwa | 10,000/= |
| 14 | Nguzo za miti ya asili | 5% ya mrahaba wa tozo ya Wakala wa Misitu Tanzania. |
| 15 | Ushuru wa miche ya miti ya kupanda | 40/= kwa mche mmoja |
| 16 | Ushuru wa nguzo za miti ya mikoko | |
| | Sentimita 15 hadi 20 | 1,500/= kwa nguzo moja |
| | Chini ya sentimita 15 | 1,000/= kwa nguzo moja |
| 17 | Miche ya mapambo | 200/= kwa mche mmoja |
| | Miche isiyo ya mapambo | 80/= kwa mche mmoja |
| 18 | Ushuru wa mazao ya mifugo na uvuvi | |

| | | |
|---|---|---|
| | a)Ushuru wa samaki kuanzia kg 30 | 10,000/= kwa kila kg30 |
| | b) Ushuru wa dagaa | 3,000/= kwa ndoo ya lita 20 kila ndoo |
| | c) Samaki wa mapambo | 50/= kwa samaki mmoja au 20,000/= kwa tenki moja. |
| 19 | A: Ada za leseni za uvuvi | |
| | Leseni za uvuvi | 20,000/= kwa raia kwa mwaka |
| | | Dola 10 kwa wasio raia kwa mwaka |
| | B: Ada za Leseni za Vyombo vya Uvuvi | |
| | a) Leseni ya mtumbwi | 20,000/=kwa mwaka |
| | b) Leseni ya boti | 30,000/=kwa mwaka |
| 20 | Ushuru kwa nguzo za miti ya kupandwa na Halmashauri kwa miti laini yote isipokuwa jamii ya *juniperus procera*: - | |
| | a) Zaidi ya sentimeta 10 dbh | 2,000/= kwa nguzo |
| | b) Kipenyo cha sentimeta 10 na chini ya hapo | Itauzwa kama kuni. |
| 21 | Ushuru wa Usafirishaji wa Madini | |
| | a) Madini ya ujenzi (mawe, mchanga, kokoto na kifusi) | 1,000/= kwa tani moja |
| | b) Usafirishaji madini (Makaa ya mawe, kopa na madini mengine) | 1500/= kwa tani moja. |
| 22 | Ushuru wa Hewa Ukaa | |
| | a) Ikiwa umiliki wa msitu ni wa Halmashauri | 61% ya mauzo ya hewa ukaa |
| | b) Ikiwa umiliki ni wa Mamlaka nyingine ndani ya Wilaya | 10% ya mauzo ya hewa ukaa |
| | c) Ikiwa umiliki ni wa mtu binafsi au vikundi vya kijamii | 4% ya mauzo ya hewa ukaa |

SEHEMU K:
I: ADA YA UPIMAJI NA IDHINI YA UJENZI

| Na | Aina ya Jengo | Kiwango cha Ada (shilngi) |
|---|---|---|
| 1 | Makazi chini ya $400m^2$ | 1,360/= |
| 2 | Makazi zaidi ya $400m^2$ | 4,240/= |
| 3 | Viwanda na biashara | 3,000/= kwa $m^2$ |
| | Maeneo mengine (huduma za jamii | 720/= kwa $m^2$ |

II: KIBALI NA IDHINI YA UJENZI

| Na | Aina ya Jengo | Kiwango cha Ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za makazi ya kawaida | 30,000/= kwa kibali |
| 2 | Nyumba za makazi na biashara | 50,000/= kwa kibali |
| 3 | Kituo cha mafuta | 200,000/= |
| 4 | Majengo ya ghorofa | 300,000/= |

*Tangazo la serikali Na.811 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Majengo ya biashara | 50,000/= |
| 6 | Minara ya simu (Telephone towers) | 300,000/= |
| 7 | Mmajengo ya ofisi binafsi | 100,000/= |
| 8 | Maghala na bohari | 200,000/= |
| 9 | Uzio | 20,000/= |
| 10 | Majengo mengineyo | 20,000/= |

SEHEMU L:
ADA YA MABADILIKO YA MATUMIZI YA ARDHI

| Na | Aina ya Jengo | Kiwango cha Ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Makazi kuwa biashara au makazi na biashara | 20,000/= |
| 2 | Makazi kuwa viwanda | 30,000/= |
| 3 | Biashara kuwa viwanda | 30,000/= |
| 4 | Makazi kuwa housing estates | 30,000/= |
| 5 | Kugawa kiwanja au shamba | 25,000/= |
| 6 | Kuhakiki hati miliki | 25,000/= |

SEHEMU M:
ADA YA KUTENGENEZA VYOMBO VYA MOTO VYA WATU BINAFSI KATIKA KARAKANA YA HALMASHAURI

| Na | Aina ya matengenezo | Kiwango cha Ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Kubomoa, kushusha na kurudishia injini ya greda, trekta na mitambo mingine | 200,000/= |
| 2 | Kubomoa, kushusha na kurudishia injini ya gari kubwa zaidi ya tani mbili | 150,000/= |
| 3 | Matengenezo ya kawaida ya greda, trekta na mitambo mingine | 100,000/= |
| 4 | Matengenezo ya kawaida kwa gari zaidi ya tani mbili | 80,000/= |
| 5 | Kubomoa, kushusha na kurudishia injini ya gari chini ya tani mbili | 80,000/= |
| 6 | Matengenezo ya kawaida kwa gari chini ya tani mbili | 40,000/= |
| 7 | Pikipiki na bajaji (matengenezo aina zote) | 25,000/= |

SEHEMU N:
ADA NYINGINEZO

| Na | Aina ya Ada | Kiwango cha Ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Choo cha umma cha kulipia | 200/= kwa mtu |
| 2 | Huduma ya bafu ya umma | 500/= kwa mtu |
| 3 | Ada ya maombi ya zabuni | 10,000/= |

*Tangazo la serikali Na.811 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Ada ya ununuzi wa zabuni kwa mradi wa zaidi ya milioni 50 | 100,000/= |
| 5 | Ushuru wa vyuma chakavu kwa tani moja | 10,000/= |
| 6 | Kibali cha kuonesha sinema (video) | 10,000/= kwa siku |
| 7 | Kibali cha kuonesha mieleka, maigizo, sarakasi, ngumi na michezo mingine | 10,000/= kwa siku |
| 8 | Ushuru wa nyumba za kulala wageni | 10% ya mtu aliyelala kwa siku |
| 9 | Mama Lishe, Baba Lishe/wauzaji vileo/nyama choma/vyombo na bidhaa nyingine mchanganyiko mnadani. | 500/= kwa siku |
| 10 | Ada ya usajili wa vikundi vya Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu | 30,000/= kwa kila kikundi |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwamba Tarehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya ……..ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi ......................... kama faini ya kufifilisha kosa na kiasi cha shilingi ..................... ambacho ni ada au ushuru ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: .....................................................
Saini: ...................................................

MBELE YA:
Jina……...............................................
Wadhifa: .............................................
Saini: ..................................................
Tarehe: ...............................................

Nembo ya. Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani lililopitishwa tarehe 12/8/2023 na ubandikaji huo kushuhudiwa na:-

SUNDAY NDORI DEOGRATIUS,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*LUDEWA*

WISE CHARLES MGINA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*LUDEWA*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
10 Agosti, 2024

Mohamed Omary Mchengerwa (MB.),
*Waziri wa Mchi-OR-TAMISEMI*